*Machakos University Journal of Science and Technology, ISSN2707-6741 Vol. 4, Issue 1, September 2024*

# Mitandao ya Kijamii, Mkenya "Mwasi" katika X, hapo awali Twitter, na Mijadala ya Uana, Jinsia na Ngono

Virginia Mwathi [1], Larry Ndivo [2]

[1,2] Idara ya Isimu na Lugha, Chuo Kikuu cha Machakos, Kenya

Ikisiri

Mitandao ya kijamii imekuwa ikitumika sana kama vyombo vya mawasiliano na utangamano miongoni mwa watu katika ulimwengu wa sasa. Kando na kutupa uhuru wa kusambaza maoni yetu, mitandao ya kijamii imewezesha watu wengi kutoa maoni yao kuhusu masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa hata kuliko zamani. Habari nyingi zinazosambazwa katika mitandao hii hazidhibitiwi kwa vile zinatokana na fikra za kibinafsi, mihemko na makabiliano ama majibu ya papo hapo ambayo inaweza kuwa yenye mapendeleo. Kutokana na haya, makala hii ilichanganua jumbe teule za mwanamtandao Mkenya maarufu aitwaye Eric almaarufu Amerix katika mtandao wa X, (hapo awali Twitter), akijitambulisha kama @Amerix. Ilitathmini kauli zake kwa kuhusisha nadharia za ubabedume na ufeministi. Kwa maoni yetu, tunadai kuwa @Amerix amechukua nafasi hii ya kuwepo kwa pengo la kijinsia linalodumu kushughulikia masuala ya 'wanaume' lakini kwa upande mwingine, tungependa kuonyesha kuwa inawezekana kuwa shughuli zake zimedhoofisha maendeleo ambayo yalikuwa yashapatikana katika kuumbua mifumo ya kiubabedume katika mpito wa wakati. Data ilikusanywa kwa usampuli wa kimakusudi ambapo jumbe teule zilizopata majibu mengi, zikasambaa sana na hata kupendwa zilitumika. Jumbe zilizoteuliwa ni zile zenye kuibua umaarufu kutokana na nembo ya hashtag #MasculinitySaturday inayotokana na vipindi vya @Amerix vya Jumamosi na kusababisha wafuasi wake wengine kumtuhumu kama anayeendeleza itikadi za kiubabedume. Utafiti huu ulibaini kuwa @Amerix ni mwenye taasubi ya kiume kutokana na anavyotetea masuala ya kiume. Aidha, ilidhihirika kuwa ni 'mwasi' kwa vile anapinga baadhi ya tamaduni ambazo zimekuwepo na hata maendeleo ambayo yalikuwa yashapatikana katika kuleta usawa wa kijinsia. Tunapendekeza watafiti wa baadaye kuchunguza namna majukwaa mengine yanavyoshughulikia suala la kijinsia. Pia, wanaweza kutoa suluhu la udunishaji wa jinsia moja. Tunatumai kuonyesha kuwa mitandao ya kijamii inatoa kipera ibuka cha mahusiano ya kifasihi na kutokana na hayo, kukutana kwa ubunifu na mijadala ya kifasihi.

Istilahi muhimu: mitandao ya kijamii, 'uume sumu' ufeministi, mfumo wa uume, udenguzi

## UTANGULIZI

Mtandao wa kijamii ni mfumo wa mawasiliano ya kielektroniki unaopitia katika kompyuta ulimwenguni unaotumiwa kutafuta taarifa, kuwasiliana na kupeana taarifa (TUKI, 2004: 280).

Maelezo haya yanaonyesha kuwa mtandao wa kijamii umeleta mahusiano ulimwenguni ambapo watu kutoka pembe tofauti za ulimwengu hutangamana kwa njia ya kielektroniki. Upekee wa mtandao huu ni kuwepo kwa utangamano huu na zaidi ya yote, uhuru wa mtumizi wake kutoa habari, mawazo, mihemko, na hata matamanio yake. Kando na hayo, watu huutumia kama jukwaa ama soko la kutangazia bidhaa na huduma zao. Vilevile, umesaidia watu kuunganishwa na marafiki wao wa zamani na hata kuunda marafiki na mahusiano mapya. Baadhi ya 'majukwaa' ya mtandao ya kijamii yanayotumika sana kuwaunganisha watu ni kama vile: Facebook, Instagram, X (hapo awali Twitter), LinkedIn, Tiktok, Telegram na kadhalika.

Katika makala hii, tulijikita katika mtandao wa X mbapo, kutokana na uhuru ambao mtumizi wa mtandao huu anao wa kuelezea habari na mawazo yake, tulichanganua jumbe teule za mwanamtandao Mkenya maarufu aitwaye Eric almaarufu Amerix. Yeye hujitambulisha kama @Amerix katika mtandao huu. Tuliamua kuchagua mtandao wa X na kuchambua jumbe kwa mkondo wa kifasihi kwa vile tunaamini kuwa mtandao huu ni kipera ibuka cha fasihi kwa vile kina sifa ya kifasihi ambayo ni kutumia lugha kwa usanii na kuwasilisha suala fulani kwa njia inayoathiri, kugusa na kuacha athari fulani kwenye hadhira. Sifa hii ndiyo inayompa @Amerix uhuru (ushatajwa) wa kuzungumzia masuala ya kijinsia. Kwa kuhusisha nadharia za Ufeministi na Ubabedume, tulitathmini kauli zake zinazomchora kama mwenye taasubi ya kiume. Taasubi ya kiume ni dhana inayotumiwa kueleza na kuhusishwa na wanaume ambao wanaipendelea na kuikweza jinsia yao huku wakiidhalilisha ile ya kike. Hii ni sifa muhimu na ya kawaida katika itikadi ya ubabedume. Taasubi ya kiume ni moja kati ya sifa nyingi zinazoshambuliwa na wafuasi wa Ufeministi (Wamitila, 2003: 209).

Wafula na Njogu (2007: 90), wanadai kuwa nadharia ya Ufeministi hupigania haki za wanawake katika jamii ya ubabedume. Wanadai kuwa mhimili mkuu wa nadharia hii ni kubaguliwa kwa wanawake katika jamii kwa misingi ya jinsia yao ya kike. Matokeo yake ni wao kuwa miongoni mwa wanyonge katika jamii. Beauvoir (1949) katika Kimondiu (2019:18) anashambulia asasi ambazo zinachangia katika ukandamizaji wa mwanamke ambazo ni ndoa na utamaduni. Anaishambulia mielekeo ya utamaduni ya kumfanya mwanamume kama kaida au binadamu-kielelezo na kumchora mwanamke kama kitu hasi na duni. Katika makala hii, mhimili mkuu wa

nadharia ya ufeministi uliotuongoza ni: jamii huongozwa na mfumo wa kiubabedume umwekao mwanamume kama msingi mkuu katika jamii na uliopangwa kwa njia inayomdunisha mwanamke katika nyanja zote za kiutamaduni zikiwemo: famila, dini, siasa, uchumi, jamii na kadhalika (Yanni, 1995:37). Vilevile, malengo mawili ya uhakiki wa kifeministi yalituongoza ambayo ni: kuziangalia upya kazi zilizoandikwa na wanaume kwa mtazamo wa kike. Kwa mujibu wa Maggie (1986) katika Osoro (2003:13), uhakiki wa kifeministi ni uchunguzi kuhusu usawiri wa kijinsia na itikadi katika fasihi kwa mtazamo wa kike. Pili, ni kuchunguza jinsi lugha inavyotumiwa kuashiria mambo mbalimbali katika fasihi.

Tunaamini kuwa, lugha ya kifasihi hutumika kusawiri mambo mbalimbali kuliko jinsi lugha hiyo inavyoweza kutumika katika miktadha isiyo ya kifasihi.

Nadharia ya ubabedume, kwa mujibu wa Wamitila (2003:241) ni dhana inayotumiwa kuelezea mfumo wa kijamii unaomtukuza mwanamume huku ukimdhalilisha au kumdunisha mwanamke. Ni mfumo unaomfanya kaida kuu ya kijamii. Huzichukulia amali za kiume na mawazo yao kama kaida za kufuatwa katika jamii nzima. Connell (2005) katika Kibigo (2020:27) anadai kuwa, ubabedume hutazamwa kwa njia zaidi ya moja kama vile mahusiano ya kijinsia, ukatili, malezi na kadhalika. Huu ndio mkondo tutakaotumia kudhihirisha ubabedume katika jumbe teule. Hii ina maana kuwa, ubabedume si sawa na nguvu za kimwili bali ni matendo ya wanaume ya kijamii. Mhimili mkuu utakaotuongoza katika utafiti huu ni ule unaojikita kwenye sifa za ubabedume. Ni sifa ambazo sharti mwanamume awe nazo ili kuweza kujenga, kudumisha na kudhihirisha ubabe. Sifa hizi ni kama vile: uvumilivu, uwezo, kutoogopa, kuthubutu, ukware miongoni mwa sifa nyingine (Kibigo, 2020:28).

## Suala la Utafiti

Majukwaa ya mtandao wa kijamii yamekuwa yakitumika kama vyombo vya mawasiliano na utangamano miongoni mwa watu katika ulimwengu wa sasa. Majukwaa haya yamewezesha watu kutoa maoni yao kuhusu masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa hata kuliko zamani. Habari nyingi zinazosambazwa katika majukwaa haya hazidhibitiwi kwa vile zinatokana na fikra za kibinafsi, mihemko na makabiliano ama majibu ya papo hapo ambayo yanaweza kuwa yenye mapendeleo. Kutokana na uhuru huu wa kutumia majukwaa haya, makala hii ilichanganua jumbe

teule za mwanamtandao Mkenya maarufu aitwaye @Amerix (keshatajwa) zinazomchora kama 'mwasi' na mwenye taasubi ya kiume.

Sababu za kuchagua Mada, Malengo ya Utafiti na Usampulishaji

Suala la jinsia, uana na ngono limeenea katika jamii tuliyomo. Limekuwa na athari miongoni mwa wanajamii katika nyanja za kiuchumi, kijamii na siasa. Hivyo, mtafiti aliteua suala hili ili kuchunguza maoni na msimamo wa mwanamtandao mwanamume ya jinsia, uana na ngono. Aidha, kwa vile suala la wanawake limeshughulikiwa na watafiti kama vile Kimondiu (2019), aliyechunguza "Usawiri wa Mwanamke katika Nyimbo za Sifo za Wakamba," naye Kibigo akachunguza suala la ubabedume katika miviga ya Shilembe na Mchezasili, ndipo nasi tukaona tuchunguze suala la ubabedume tukijikita katika mtandao wa X.

Malengo mawili yaliongoza utafiti huu ambayo ni mwanzo, kumchora @Amerix kama mwenye taasubi ya kiume na pili, kudhihirisha mtandao wa kijamii kama kipera ibuka cha fasihi kinachoweza kuzungumzia masuala muhimu ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Usampuli ulikuwa wa kimakusudi ambapo jumbe teule zilizozungumzia masuala ya kijinsia, zikapata majibu mengi, zikasambaa sana na hata kupendwa zilitumika. Jumbe zilizoteuliwa ni zile zenye kuibua umaarufu kutokana na nembo ya hashtag #MasculinitySaturday.

MBINU ZA UKUSANYAJI WA DATA NA MATOKEO YA UTAFITI

Utafiti ulikuwa wa maktabani ambapo tulihakiki jumbe katika mtandao wa X. Jumbe hizi ndizo zilizokuwa data ya msingi. Jumbe zilizohakikiwa ni zile zilizozungumzia masuala ya jinsia, uana na ngono. Data ya upili ilipatikana kwa kusoma vitabu, makala na tasnifu za watafiti wengine zenye uhusiano na mada teule. Vifaa vilivyotumika katika utafiti huu ni vifuatavyo: kipakatalishi, daftari, kalamu na rununu. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa njia ya uchanganuzi maelezo.

Utafiti ulipata @Amerix ni 'mwasi' na mwenye taasubi ya kiume. Vilevile, tulibaini kuwa mtandao wa kijamii ni kipera ibuka cha fasihi. Tumejadili ifuatavyo.

UBABEDUME UNAVYODHIHIRIKA KATIKA JUMBE TEULE ZA X ZA @AMERIX

Katika uainishaji wa jumbe za @Amerix kwenye mtandao wa X, tuligundua kuwa, jumbe hizi zimemchora kama mwenye taasubi ya kiume kwa njia tofauti. Tofauti hizi zinatokana na kuainisha jumbe ifuatavyo: zinazoonyesha mapendeleo kwa mwanamume, zinazomhimiza mwanamume kuwa msingi mkuu na kaida kuu katika jamii, zinazomdunisha mwanamke kwa njia ya moja kwa moja, zinazomdunisha mwanamke kwa njia isiyo ya moja kwa moja na zinazomchora @Amerix kama mwasi.

Ni kweli kusema kuwa, @Amerix ametumia nafasi hii ya kuwepo kwa pengo la kijinsia linalodumu katika jamii kushughulikia masuala ya wanaume. Ametumia mtazamo wa kijamii kuwa jinsia ya kiume imepuuzwa kama jukwaa la kuandika jumbe zinazohuzu kushauri urejeshaji wa ubabedume uliokuwa umeanza kufifia kutokana na upiganiaji wa usawa wa kijinsia. Tunakisia kuwa, matatizo ya kijamii kama vile ripoti za mauaji ya wanawake, kuvunjika kwa ndoa nyingi na malezi mabovu ya watoto ni mazao ya kufa kwa ubabedume ambao @Amerix anapigania kurejeshwa kwake.

Mapendeleo kwa mwanamume

Kwanza, katika kumchora @Amerix kama mwenye taasubi ya kiume, tumechambua matumizi yake ya lugha na uteuzi wa hadhira yake. Tumegundua kuwa, tabia ya kuelekeza jumbe zake kwenye jinsia ya kiume inaonyesha kuwa kwa namna fulani, anapuuza ile ya kike. Hii ni licha ya kuwa jumbe zake zingine zinaweza zikawafaa wanawake hasa zinazogusia masuala ya afya, uchumi na jamii lakini inatokea kuwa anapendelea jinsia ya kiume. Hii inaonyesha kuwa, anaiona jinsia ya kike kama isiyo na thamani yoyote au yenye thamani duni sana katika jamii. Ujumbe wake wa tarehe 26/03/22 unasema kuwa,

"Men, here are enemies of men, -

Masturbation - Pornography -

Obesity/Fatness - Betting & gambling - Alcoholism - Prostitution - Smoking - Sugar & seed oils - Lack of sleep. Stay away from these enemies. Your loved ones depend on you for survival.

#MasculinitySaturday"

"Wanaume, haya ndiyo maadui ya wanaume: punyeto, filamu za ngono, wizani kupita kiasi, uchezaji kamari, ulevi, ukahaba, uvutaji wa sigara, sukari mafuta ya mbegu na ukosefu wa usingizi. Wapendwa wako wanakutegemea ili kuishi."

Ujumbe huu unampa wosia mwanamume njia ya kulinda afya yake. Anaonyeshwa vitabia vinavyoweza kuidhoofisha afya yake na kushauriwa kujiepusha navyo. Kwa maoni yetu, huu ni ujumbe ambao ungefaa hadhira ya jinsia zote mbili kwa vile hivi vitabia pia huathiri mwanamke. Mwanamke ana afya anayofaa kulinda pia. Vilevile, inatokea kuwa amechora mwanamume kama tegemeo la familia. Kwa kusema kuwa, “Wapendwa wako wanakutegemea ili kuishi,” inaonyesha kuwa pasipo mwanamume, familia haiwezi kudumu. Amewachora wanawake na watoto kama wategemezi ijapokuwa katika maisha ya sasa, wanawake wengi wamechukua jukumu la kulea watoto kibinafsi. Rais wa Kenya alitaja suala hili la ulezi wa watoto kibinafsi katika sherehe za Madaraka mnamo tarehe 01/06/22. Akadai kuwa visa kama hivi vimeongezeka kutoka asilimia ishirini na tano nukta moja hadi asilimia thelathini na nane nukta tisa (25.1%-38.9%) kati ya miaka ya 2009-2019. Tunakisia kuwa, idadi kubwa ya visa vya ulezi wa kibinafsi ni ile ambayo mwanamke ndiye anayechukua jukumu la ulezi.

Tarehe 25/03/2022, @Amerix alisema,

“Men, TV news is propaganda, its content: Diseases - Disasters - Distraction – Deaths. It is designed to emasculate the man & weaken the mind. Protect your mind from Media's 4Ds. Read books, journals & periodicals to build a resilient mindset. #MasculinitySaturday”

“Wanaume, habari za televisheni ni propaganda. Zina : magonjwa, mikasa, vifo. Zimeundwa kumdhoofisha mwanaume na akili yake. Ilinde akili yako kutokana na yaliyo katika mtandao huu. Soma vitabu, majarida na magazeti ili kuunda akili yenye nguvu.”

Katika ujumbe huu, mwanamke ametengwa. Televisheni ni chombo kinachotumika na jinsia zote mbili. Suala la kuzingatia mwanamume moja kwa moja kwenye ujumbe huu linaweza kufasiriwa kama mbinu ya kumtenga mwanamke katika ushauri ambao ni bora kwa jinsia zote mbili na hivyo tabia hii inamchora @Amerix kama binadamu ambaye hamthamini mwanamke. @Amerix anaendelea kusema kuwa,

"Men, when life gets bad, Get hard! When setbacks and hardships punch you hard, it is an opportunity to punch back harder, Don't allow victim mentality to take over, Get up and punch harder. A man becomes better. When things become bad. #MasculinitySaturday"

"Wanaume, maisha yanapokuwa mabaya, kuwa mgumu! Vikwazo na Magumu yanapokuandama kwa mpigo, ni nafasi yako kujikaza zaidi. Usiruhusu mafikira ya unyonge kukutawala, inuka na ujikaze zaidi. Mwanamume huwa bora zaidi mambo yanapoharibika."

Kwa kawaida, maisha huwa magumu kwa jinsia zote mbili. Kwa kweli, ushauri huu, ungefaa jinsia zote mbili. Tendo la kuuelekeza kwa hadhira ya wanaume kunaonyesha namna anavyomthamini mwanamume katika maandishi yake na hivyo kuna uwezekano kwamba @Amerix anapuuza wanawake. Tunaonelea kwamba, mtazamo wa @Amerix unafaa kuhusisha hadhira ya jamii kwa jumla pasipo kutenga jinsia yoyote kwani majukumu ya jamii, shida zinazokabili binadamu na jinsi ya kutatua matatizo ni jukumu la kila mmoja wetu.

Kuanza taarifa zake kwa kusema, "Men (wanaume)" na kumalizia kwa #MasculinitySaturday (Jumamosi ya uume) kunaonyesha wazi namna anavyochukulia kwa uzito suala la kumwinua mwanamume. Kunaonyesha pia anavyojitia hamnazo kuhusiana na maendeleo ya mwanamke. Tabia ya kulenga wanaume tu kama hadhira yake kunaleta mtazamo uliokitwa kwenye msingi wa fikra za kiume kuwa mazungumzo muhimu yanafaa kuelekezwa kwenye hadhira ya wanaume na hivyo basi kutenga wanawake na kusababisha kubaguliwa kwao. Wafeministi wamepigania usawa wa kijinsia katika masuala ya kiafya, kisiasa, kijamii na kiuchumi kwa kudai kuwa jinsia zote ni sawa. Kwa maoni yetu, katika utoaji wa ushauri kuhusiana na masuala mbalimbali ya maisha, @Amerix angelenga jinsia zote mbili kuwa hadhira yake.

Mwanamume kama msingi mkuu na kaida kuu katika jamii

Nadharia ya ubabedume inachukulia amali za kiume na mawazo yao kama kaida za kufuatwa katika jamii nzima (Wamitila, 2003:241). Ubabedume hutazamwa kwa njia zaidi ya moja kama vile: mahusiano ya kijinsia, ukatili, malezi na kadhalika, (Connell, 2005) katika Kibigo (2020:27). @Amerix ameshikilia haya kwa uzito. Mnamo tarehe 26/3/22, alisema,

"Men, a true man must scatter his seeds. Your scrotum carries 4 generations. Scatter them. If you attend a true man's funeral, you will see newer children being introduced. Why? Because a man does not walk around with one headlamp like a motorcycle. #MasculinitySaturday"

"Wanaume, sharti mwanamume wa kweli asambaze mbegu zake. Uzazi wako hueba vizazi vinne. Zisambaze.

Unapohudhuria mazishi ya mwanamume wa kweli, utaona watoto wageni wakitambulishwa. Kwa nini? Kwa sababu mwanamume hatembei na taa moja kama pikipiki."

Ujumbe huu unamhimiza mwanamume kuwa mkware. Kwa kusema kuwa, "…mwanamume wa kweli sharti asambaze mbegu zake," na kuendelea kusema, "…hatembei na taa moja kama pikipiki," ni mbinu ya kumhimiza kuwa mkware. Kwa hivyo, kushauriwa kutotembea na tochi moja ni lugha yenye fumbo. Anaelezwa kuwa anafaa kuwa uhusiano na mwanamke zaidi ya mmoja. Atafanya haya ili kudhihirisha ubabe. Ukware ni moja ya sifa za kiubabedume anazozizungumzia Kibigo (2020:28). Kwa mujibu wa Chiramaoke (2005:141), kiungo cha dhakar kifanye kazi. Kiweze kupenyeza na mwenye uhusiano wa ngono na kimapenzi zaidi ya mwanamke mmoja nje ya ndoa. Kwa hivyo, nadharia hii hufungamanishwa na dhakar au uume na mwenye kuimiliki. @Amerix anaendelea kudokeza,

"Men, people are not equal and shall unequal as possible. Remain at the top never be equal. So, in a relationship, always. The moment you will try to never level the field. Make it as level the field, she will conquer you,

lose interest and dump you. #MasculinitySatuturday.

"Wanaume, watu si sawa na hawatawahi kuwa sawa. Kwa hivyo,

katika mahusiano, usiwahi ruhusu uwanja uwe sawa. Ufanye usiwe sawa kadri ya uwezo wako. Daima kuwa juu. Punde tu utakaporuhusu uwe sawa, mwanamke atakushinda, apoteze hisia zake kwako na akuache."

Katika ujumbe huu, mwanamume anahimizwa kuwa daima juu ya mwanamke katika mahusiano yao. Awe ndiye wa kufuatwa. Hii ni sifa kati ya zingine alizozitaja Kibigo (2020:28), ambazo mwanamume anafaa kuwa nazo ili aweze kujenga na kudumisha ubabe. Sifa hizi ni kama vile: uwezo, kuthubutu, kutoogopa miongoni mwa zingine. @Amerix amemchora mwanamke kama ambaye daima anafaa kuwa chini ya mwanamume na anayehitaji mwongozo wa mwanamume katika kila jambo maishani. Anamwona mwanamke kama aliye daima kwenye ushindani na mwanamume na hivyo sharti adumishwe kwenye hadhi ya chini kuliko mwanamume katika nyanja zote za maisha. Mtazamo wa @Amerix katika ujumbe huu kuhusu wanawake ni kuwa mwanamke ni mjanja na aliyejawa na nia ya kumwondoa, kumharibu na kumtawala mwanamume. Hapa ni anaposema kuwa, "Punde utakaporuhusu uwe sawa, mwanamke atakushinda, apoteze hisia zake kwako na akuache." Kwa maoni yetu, madai haya si ya kweli kwa vile Ufeministi unapigania usawa wa kijinsia na uthamini wa uwezo walio nao wanadamu bila kubagua jinsia. Vilevile, inawezekana kuwa wapo wanaume wengine wanaoweza kuwa na sifa ambazo @Amerix anawapa wanawake ikiwa majukumu yangepinduliwa.

Katika suala la uzazi, @Amerix anashauri ifuatavyo,

"Men, be in charge of conception. Do not allow your woman to dictate how many babies she wants. Take control of your sperms because it is you who will shoulder the burden of responsibility, NOT her. Let her cry as she wants, but guard your seeds.

"Wanaume, kuwa mdhibiti wa uzazi. Usimruhusu mkeo kutoa uamuzi wa idadi ya watoto ambao angependa. Dhibiti manii yako kwa vile wewe ndiye utakayebeba mzigo wa kuwajibika, SI yeye. Acha alie namna atakavyo, lakini linda mbegu zako.

#MasculinitySaturday"

Ujumbe huu unaonyesha kuwa, mwanamke hana uhuru wa kutoa uamuzi ama maoni katika suala la uzazi na ulezi. Mwanamume anahimizwa kuwa ndiye anayefaa kudhibiti uzazi. Daima, mwanamke awe ndiye anayefuata maoni na maagizo ya mumewe kuhusiana na uzazi. Mwanamke amechorwa pia kama asiye na uwezo wa kiuchumi wa kulea kwa kusema, ".... wewe ndiye utakayebeba mzigo wa kuwajibika, SI yeye." Kwa maoni yetu, kwa kuandika 'SI' kwa herufi

kubwa, kunaonyesha ama kusisitiza namna mwanamke anavyodunishwa na kutengwa katika suala la ulezi. Kwa hivyo, mwanamke amechorwa kama chombo cha kuzaa tu huku mwanamume akichorwa kama mwenye kukimu na kutosheleza mahitaji ya familia. Hii ikiwa sifa inayofungamanishwa na ubabedume (Walsh, 1997) katika Kibigo (2020:34). Ifahamike kuwa, katika uzazi, jinsia zote ni sawa kwa vile, mwana haji bila jinsia hizi mbili kujamiiana. Vilevile, mwanamke pia ana uwezo wa kukimu mahitaji ya familia. Momanyi (2002) katika Kimondiu (2019:33), anadai kuwa, wanawake halisi wanatekeleza majukumu mengi muhimu ambayo hubainisha vipawa vyao. Vipawa hivi ni kama vile kukidhi mahitaji ya mume na yale ya watoto kama vile: upishi, usafi, utoaji wosia, na kadhalika, kuajiriwa na kuchangia kukua kwa nchi kiuchumi, uongozi wa kisiasa na kwenye makampuni ya kiserikali, ya kijamii na yale ya kibinafsi

Kutokana na matamshi ya @Amerix, yanavyomhimiza mwanamume kuwa msingi mkuu na kaida kuu katika jamii, tunakubaliana na maoni ya Walsh (1997) katika Kibigo (2020:34) kuwa, mwanamume hazaliwi na uume kama sehemu ya viungo vyake bali hujengwa na kukuzwa na utamaduni anamokulia. Tunaamini kuwa, juhudi za @Amerix za kurejesha ubabedume zinamfanya apuuze majukumu ya wanawake na mchango wao katika jamii.

Usawiri wa mwanamke

Katika uchambuzi wa jumbe za @Amerix, tumegundua kuwa amemchora mwanamke kwa njia hasi. Anamdunisha kwa njia ya moja kwa moja na kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Mogere (2003) anadai kuwa, usawiri wa wahusika wa kike katika fasihi ya Kiswahili una utata mwingi kufikia sasa. Inadaiwa kwamba, wanawake wanasawiriwa kwa njia isiyofaa hasa katika kazi zilizoandikwa na wanaume. Mwanamume anapoandika kazi ya kifasihi, huwaonea wanawake na kuwasawiri wahusika wa kike kwa njia isiyopendeza huku akiwapendelea wahusika wa kiume. Inadhihirika kuwa, @Amerix kama mwanamtandao wa kiume, amemchora mwanamke kwa njia hasi. Katika sehemu hii, tutachunguza jumbe zake kuhusu usawiri wa kijinsia na itikadi katika fasihi kwa mtazamo wa kike, hili likiwa ni moja kati ya malengo ya uhakiki wa kifeministi.

Kudunishwa kwa mwanamke kwa njia ya moja kwa moja

@Amerix ametumia mbinu hii kumchora mwanamke kama kiumbe duni. Anamweleza mwanamume kuhusu uhasi wa mwanamke kwa uwazi. Hii inadhihirika kutokana na jumbe zifuatazo:

"Men, it's very easy to con career women, they think their cars, money & stilettos attract men, a sly man with a hired car & a borrowed suit will easily slide into her pants & wallet. Career women are weaker, make wrong choices & unknowingly date thugs. #MasculinitySaturday."

magari, pesa na viatu vyao vya kuchuchumia huvutia wanaume. Mwanamume mjanja aliyekodisha gari na kuomba suti ataingia kwenye suruali na kibeti chake kwa urahisi. Wanawake kama hawa ni dhaifu, hufanya uamuzi usiofaa na hata kuingia kwenye mahusiano ya kimapenzi na wahuni.

Wanaume, ni rahisi sana kulaghai wanawake wenye kazi.

Wao hudhani

Ujumbe huu unaonyesha namna mwanamke aliyejikomboa kiuchumi anavyodunishwa. Ni kweli kusema kuwa, katika ujumbe huu, @Amerix amemchora mwanamke kama mtu mjinga kwa vile hata baada ya ya kujikomboa kiuchumi, ni rahisi kwa mwanamume mjanja na mwenye nia mbaya kupenya kwenye suruali na kibeti chake. @Amerix anamwona mwanamke kama mwepesi wa kulaghaiwa na kudhibitiwa ili atosheleze matamanio ya mwanaume licha ya kiwango chake cha elimu na uwezo wake wa kiuchumi. Kwa upande mwingine, mwanamume amechorwa kama mjanja na mwenye busara ya maisha, mwenye uwezo wa kumtumia mwanamke katika harakati zake za kibinafsi. Kwa hivyo, mwanamke amechorwa kama mwenye elimu ya kazi yake tu bali si ya maisha kwa jumla. Kusema kuwa mwanamume anaweza kulaghai mwanamke kwa suti ya kuomba na gari la kukodisha tu kunaonyesha kuwa mwanamke ni mwepesi wa kudanganywa. Anayeona uzuri wa kitu wa nje tu bali si wa ndani. Ujumbe huu unaonekana kupinga na kukinzana na maoni ya Woolf (1929) katika Kimondiu (2019 :103) anayelipa uzito suala la uchumi katika ukombozi wa mwanamke. Kulingana na Woolf, mwanamke hawezi kupata ukombozi wa aina yoyote kama hajakombolewa kiuchumi. Kwa hivyo, kuchorwa kwa mwanamke afanyaye kazi kama mjinga ni kumdunisha kwa njia kubwa. Uwezo wa @Amerix kuwa na ushawishi mkubwa kwa wafuasi wake kunawawezesha hasa wale wa kiume kudunisha mwanamke wanapoeleza sifa

za mwanamke na hivyo basi hata bila kunuia, kunafanya iwe sawa kwa wanaume kushikilia maono hayo na kumdharau mwanamke. Anaendelea kusema kuwa,

"Men, don't commit to a church girl, especially if she's above 30 years. Church girls are diabolical, duplicitous & hypocritical. When they pray, they cry so loudly because they regret wasting their 20s kneeling for blowjobs instead of kneeling for God.
#MasculinitySaturday."

"Wanaume, usimpe muda mwingi msichana aliyezamia kanisani hasa akiwa zaidi ya miaka 30. Wasichana walioshikilia kanisa huwa wanafiki. Wanapoomba, hulia kwa sauti kwa sababu wanajutia kupoteza miaka yao ya 20 walipokuwa wakipiga magoti kufanya tendo la ngono badala ya

kupigia Mungu magoti.

Ujumbe huu unaonyesha maisha ya mtu wa jinsia ya kike yakiwa mafupi; yanayokitwa na wakati sana. Kwa kusema kuwa anayezidi miaka 30 asipewe muda na mwanamume, ni kuonyesha kuwa ameshapitwa na wakati. Anamfananisha na ua ambalo sifa yake ni urembo lakini hunyauka kwa haraka. Kwa hivyo, mwanamke anaonekana kama asiye na thamani ya kudumu. Vilevile, msichana mcha Mungu anaonekana kama anayetumia sifa hii kulipiza muda wake wa hapo awali aliokuwa akiutumia kujihusisha katika ukware. Ifahamike kuwa, ikiwa alijihusisha katika ukware katika miaka yake ya 20, je, alijihusisha katika tendo hili peke yake? Jinsia ya kiume sharti iwe na mchango katika tendo hili kwa sababu, kwa kawaida, jinsia hizi mbili sharti zitangamane ili tendo hili kufanyika. Kwa hivyo, @Amerix anamwona mwanamume kama asiye na doa na kumhukumu mwanamke anayezidi miaka 30 kwa kuchelewa kuolewa. Asasi kama hizi ndizo Beauvoir (1949) anazoshambulia, zinazomkandamiza mwanamke ambazo ni ndoa na utamaduni. Tunakubaliana na maoni ya mke wa Rais mstaafu wa Taifa la Amerika, Michelle Obama aliyesema, "Wanaume wakakamavu- wanaume ambao ni vielelezo bora vya kweli, hawafai kudunisha wanawake ili kujidhihirisha kama wenye nguvu."

Katika ukuaji wa mwana wa kike, @Amerix anapendekeza,

Abolish boarding schools for GIRLS. They suppress their feminine instincts, they deny them an opportunity to appreciate masculine dominance, they destroy their natural roles in making the right life choices and damage their emotions. Few parents know this.

Ondoa shule za bweni za wasichana. Huwa zinadunisha silika zao za kike, zinawanyima nafasi ya kutambua kuwepo kwa uume, zinaharibu majukumu yao ya kiasilia katika kufanya uamuzi bora maishani na kuharibu mihemko yao. Wazazi wachache wanafahamu haya.

Ujumbe huu unaonyesha kuwa @Amerix anamwona mwanamume kama kiumbe muhimu katika ukuaji wa mwana wa kike. Hapa ni anaposema kuwa, shule za bweni za wasichana ziondolewe kwa vile zinawanyima nafasi ya kutambua kuwepo kwa uume. Anaelekea kudai kuwa sharti mwana wa kike akulie kwenye kivuli cha mwanamume kwa sababu kuna ‘sifa teule za kike’ ambazo anafaa kuzipata kutoka kwa mwanamume anaposema, “…zinaharibu majukumu yao ya kiasilia katika kufanya uamuzi bora...” Kwa kutosema shule za bweni za wavulana ziondolewe, anamdunisha mwanamke kwa vile inadhihirika kuwa, mwana wa kiume anaweza akakua vyema bila kuwepo kwa mwanamke maishani mwake lakini yule wa kike ni duni kwa vile sharti akulie kwenye kivuli cha mwanamume. Kwa hivyo, kwa uwazi, anamwona mwanamke kama atakayekuwa duni ama dhaifu akikulia kwenye mazingira ya kike tu, asiye na uwezo wa ‘kujilea’ ama hata ‘kulea’ mwenzake.

Kudunishwa kwa mwanamke kwa njia isiyo ya moja kwa moja

@Amerix ametumia mbinu hii kumchora mwanamke kwa njia hasi. Ni mbinu isiyotumia uwazi kueleza uhasi wa mwanamke. Kwa mfano, kwenye suala la malezi,

@Amerix anasema

“Men, detach your son from his mother as early as possible, send him to go play with other boys, let him learn to fight there, let him learn team-building there, let him learn creativity there, do not allow him to cling to his mother. Raise a son! #MasculinitySaturday”

“Wanaume, mtenganishe mwanao wa kiume na mamake mapema iwezekanavyo. Mtume akacheze na wanaume wenzake, wacha akajue kupigana na ufanyaji kazi kama kundi moja, apate kuwa mbunifu, usimruhusu kukaa na mamake. Lea mwana wa kiume!”

Ujumbe huu, hauonyeshi udhaifu wa mwanamke kwa uwazi lakini kutokana na uchambuzi wa ndani, inadhihirika kuwa, mwanamke anasawiriwa kama asiye na uwezo wa kulea mwana wa kiume ingawaje yeye ndiye aliyemzaa. Kwa mwana wa kiume akaaye na mamake sana, inakisiwa kuwa atakua na vitabia visivyo vya kiume, hatakuwa mwanamume. Inaonekana kuwa mwana wa kiume anapokua na vitabia visivyo vya kiume, mwanamke ndiye atakayesingiziwa.

@Amerix anaendelea kudokeza,

"Men, a father is an important pillar in the life of a woman. If a woman grew up without a father, it becomes disastrous for her. A father is a woman's first boyfriend. Before you date, find out her relationship with her father. Save yourself from chaos. #MasculinitySaturday

Wanaume, baba ni mnara muhimu katika maisha ya mwanamke. Ikiwa mwanamke alikua bila baba, atapata changamoto. Baba ni mpenzi wake wa kwanza. Kabla ya kuingia kwenye mahusiano na msichana, chunguza kuhusu uhusiano wake na babake. Jiokoe kutokana na vurugu.

Jumbe hizi zinaonyesha kudunishwa kwa mwanamke katika suala la malezi. Anaonekana kuwa asiye na mchango mkubwa katika kukua kwa mtoto. Kwa kusema kuwa, "Jiokoe kutokana na vurugu," inaonyesha kuwa mwana asiyekua bila baba mwishowe huwa mtu asiyetoshea katika jamii kwa kukosa maadili fulani ambayo ni mzazi wa kiume tu ambaye anaweza kumfunza mwana katika kukua kwake. Maoni ya @Amerix yanakinzana na ya Kasiva (2019, uk.52), anayemsawiri mwanamke kama mlezi mwema katika uchambuzi wake wa usawiri wa mwanamke katika nyimbo za sifo za Kikamba. Anamwona mwanamke kama anayehakikisha watoto wake na mumewe wamepata lishe. Watoto kumlilia mama ni dhihirisho tosha kuwa mama ni muhimu katika malezi ya mtoto. Kasiva anaendelea kusema kuwa, tendo la bwana kumrai mke wake arudi nyumbani wanapokosana ni dhihirisho tosha kuwa mama ni mnara muhimu katika familia. Kwa hivyo, kwa maoni yetu, mwanamke aheshimiwe katika familia.
Ijulikane kuwa ana mchango mkubwa katika kukua kwa watoto.

@Amerix anaongezea maongezi yake kwa kusema,

Men, do not take relationship advice from women. You will burn your fingers. Whether she is a 'professional marriage counsellor' or an 'experienced wife.' A gazelle does not teach a lion how, when, why and where to hunt.
#MasculinitySaturday

Wanaume, msipokee ushauri unaohusiana na mahusiano ya kimapenzi kutoka kwa wanawake. Mtachoma vidole vyenu. Awe ni 'mtaalam wa kutoa ushauri wa ndoa' ama 'mke mwenye tajriba', msikubali. Paa hamfunzi simba njia ya, lini, kwa nini na mahali pa kuwindia.

Ujumbe huu kwa njia isiyo wazi, unamsawiri mwanamke kama kiumbe dhaifu hasa kwa kumlinganisha na paa huku ukilinganisha mwanamume na simba. Vilevile, mwanamke anaonekana kama kisababishi cha madhara yanayomfanyikia mwanamume kwa kusema, "…mtachoma vidole vyenu." Hapa ni baada ya kupokea ushauri kutoka kwa mwanamke. Kando na hayo, mwanamke msomi na mwenye tajriba anadunishwa kwa kutopewa nafasi ya kuitumia tajriba yake @Amerix anaposema, "…awe ni mtaalam wa kutoa ushauri wa ndoa' ama mwenye 'tajriba', msipokee ushauri."

Wamitila (2002) anadai kuwa, usawiri mzuri wa wahusika hufanya wasomaji wajitambulishe nao kwa kuhisi wanavyohisi na kuwaza wanavyowaza. Kwa maoni yetu usawiri hasi wa mwanamke unaifanya hadhira kuwa na itikadi potovu kwake. Ni vyema kuonyesha sifa zake chanya. Kama Momanyi (2002) katika Kimondiu (2019:33) anavyodai, fasihi ya Kiswahili haina budi kushughulikia namna ambavyo mwanamke anaweza kuigwa kutokana na uwezo wake. Ni vyema kudhihirisha sifa zao pasi kudidimizwa kwa ule uwezo wao wa kimaumbile. Mwana wa kifalme Harry, (Prince Harry) anadai kuwa, "Tunajua kuwa wanawake wanapoinuliwa, huboresha maisha ya kila mtu katika mazingira yao, familia zao, jamii zao na nchi zao kwa njia isiyomithilika," haya ni maoni ambayo tunakubaliana nayo.

@Amerix kama mwasi

Mwasi ni mtu mwenye tabia ya kuvunja sheria au kutotaka kufuata amri (TUKI, 2004: 294). Katika muktadha huu, tumemchora @Amerix kama anayepinga masuala fulani ya kijinsia katika jamii,

anayetupilia mbali suala la usawa wa kijinsia ambao umepiganiwa na wafeministi na kufanikiwa kwa kiwango fulani. @Amerix anadai kuwa,

“A woman must respect her husband. She becomes disrespectful & disdainful, she will must respect the man that gave her join the slippery road to misfortune, motherhood. She has no choice. If she

loneliness and misery. Things won't work out for her, forever. #BetterTogether”

“Mwanamke sharti amheshimu mumewe.

Sharti aheshimu mwanamume aliyemfanya mama, hana chaguo. Mwanamke

anapokosa heshima, atafuata njia inayomwelekeza katika kutofanikiwa, upweke na shida. Hatafanikiwa katika matendo yake, milele.”

Hapa, mwanamke anaonekana kuwa daima anafaa kuwa chini ya mwanamume kihadhi. Mwanamume anaonekana kama anayestahiki heshima kutoka kwa mwanamke. Ulimwengu nao unaonekana kama wenye uwezo wa ‘kumwadhibu’ mwanamke asiyemheshimu mumewe @Amerix anaposema kuwa, “...anapokosa heshima, atafuata njia inayomwelekeza katika kutofanikiwa...” Usawa wa kijinsia umepiganiwa kwa muda mrefu na wafeministi katika nyanja za familia, dini, siasa uchumi, jamii na kadhalika na kufanikiwa kwa kiwango fulani. Mwanamke anastahiki heshima pia kutoka kwa mumewe kwa kumfanya baba kama yeye alivyofanywa mama. Wote wana mchango sawa katika uzazi. Kwa hivyo, matamshi ya @Amerix yanamsawiri kama anayepinga usawa wa kijinsia kwa kutoonyesha kuwa heshima ina uwili. Kunafaa kuwa na heshima kati ya jinsia zote mbili katika ndoa tofauti na anavyoisawiri ndoa kwa kuonyesha kuwa mwanamume anamfanyia mwanamke neema. La kweli ni kuwa maongezi yake yameelekezwa kwa mwanamume kwa njia inayomhimiza kumdunisha mwanamke.

Katika suala la dini, @Amerix anasema,

"Men, still on religion, your woman must join your religion, she should abandon her denomination for your denomination, if you go to your church while she goes to her church, you are an idiot! Or, if you are also going to her church, you are pussified!

#MasculinitySaturday"

Wanaume, bado katika dini, mke wako sharti ajiunge na dini yako, aliwache dhehebu lake aje lako. Ukienda kanisa lako huku akienda lake, wewe ni mjinga! Ama ikiwa unaenda kanisa lake, unaongozwa na uke!

Ujumbe huu unamhimiza mwanamume kuwa ndiye kiongozi wa familia na kumkashifu vikali anayefuata mienendo ya mkewe kwa kumwita "mjinga" na kumwambia kuwa anaongozwa na uke. Mwanamke anachorwa kwa chombo kinachoweza kulainishwa ili kuoana na matakwa ya mumewe. Katiba ya Kenya inampa kila mwananchi uhuru wa kidini. Uhuru wa kufuata dini aipendayo na kwenda dhehebu apendalo. @Amerix kusema kuwa sharti mwanamke ajiunge na dhehebu la mumewe kunaonyesha kuwa anapinga uhuru wa kidini walio nao Wakenya. Kwa hivyo, anaonekana kama anayedhoofisha maendeleo ambayo yalikuwa yashapatikana katika kuumbua mifumo ya kiubabedume.

Kwa kuwa na maoni yanayokinzana na utamaduni, anaendelea kuonekana kama mwasi anaposema,

Men, when your woman gives birth, make sure it is you giving a name to your baby. Your baby must own your name or the name of your ancestry. Then keep the birth certificate in your custody. Never give away this power and privilege to her.

#MasculinitySaturday

Wanaume, mkeo anapojifungua, hakikisha kuwa wewe ndiye unayempa mtoto jina. Sharti mwanao amiliki jina lako ama la ukoo wako. Kisha weka cheti chake. Usimpe mwanamke uwezo na neema hii.

Kwa kumnyima mwanamke haki ya kumpa mwana jina na kuweka cheti chake cha kuzaliwa, mwanamke anaonekana kama asiye na haki ya kummiliki mtoto. Kwa kupinga mwana asipewe jina la ukoo wa kina mwanamke, @Amerix anaonekana kuwa mwasi. Kwa kawaida, jamii nyingi za Kiafrika wana hupewa majina kutoka koo zote mbili. Kwa mfano mwana wa kiume na kike wa kwanza hupewa jina la ukoo wa kina mwanamume huku wa pili wakipewa la ukoo wa kina mwanamke. Mfano ni katika jamii ya Wakikuyu. Katika suala la utamaduni tu, anazidi kusema,

Men, avoid a wedding as much as possible, the ring is a symbol of imprisonment. A wedding is a covenant you make with the Government. Break the covenant and face the Government in court. #MasculinitySaturday

Harusi ni agano kati yako na serikali. Vunja agano hilo na ukabiliane na serikali kortini.

Wanaume, jiepushe na harusi kadri ya uwezo wako, pete ni ishara ya kifungo.

Tangu enzi za mababu zetu, harusi imekuwa ni sherehe inayounganisha mke na mume nayo pete ikiwa ni ishara ya muungano huu. Serikali pia hutambua jukumu la harusi. Ingawaje si lazima kwa mke na mume kuwa na sherehe hii wanapoamua kuoana, tendo la @Amerix kupinga harusi linaonyesha namna anavyokinzana na utamaduni. Kwa hivyo, ingawaje @Amerix anamhimiza mwanamume kuwa na ubabe, anajitokeza kama mwasi kwa kuwa na maoni yanayokinzana na utamaduni. Inawezekana msomi kumwona @Amerix kama mwenye maoni potovu ambayo yanaweza kuelekeza wanajamii kutenda isivyofaa na mwishowe kuangamia.

Uelekezaji wa usemaji wake kwa wanaume kwa njia inayowahimiza kudunisha wanawake ni ushahidi tosha kuwa anatumia mtandao wa kijamii kwa njia chanya na hivyo basi kustahiki kuitwa ‘mwanamtandao mwasi’.

## HITIMISHO

Makala hii imeonyesha mtandao wa kijamii ikijikita katika X, kama kipera ibuka cha fasihi. Imeonyesha uhuru alio nao mtumizi wa mtandao huu wa kutoa habari, mawazo, mihemko na hata matamanio yake. Tunaamini kuwa ni kipera ibuka cha fasihi kwa vile kina sifa ya kifasihi ambayo ni matumizi ya lugha kwa usanii na kuwasilisha suala fulani kwa njia inayoathiri, kugusa na kuacha athari fulani kwenye hadhira (Wamitila, 2003: 42). Ni kutokana na uhuru huu, ambapo @Amerix amechukua fursa hii na kutumia jukwaa hili la mtandao wa kijamii kushughulikia suala la mahusiano ya kijinsia. Kutokana na uchambuzi wetu wa jumbe zake, inadhihirika kuwa ni mwenye taasubi ya kiume kutokana na anavyotetea masuala ya kiume na kutowacha shauku yoyote katika

mawazo ya msomaji kuwa amejawa na masuala ya kiume yenye mapendeleo na yanayobagua wanawake. Anapozungumzia wanawake, ni kwa njia hasi inayowadunisha na kuonyesha kuwa daima mwanamke anafaa kuwa chini ya mwanamume kihadhi katika nyanja zote za maisha. Kutenga siku ya Jumamosi '#MasculinitySaturday'

(Jumamosi ya uume) ili kuwashauri wanaume na kuanza jumbe zake kwa kusema, "Men" (Wanaume) kunadhihirisha namna anavyopendelea jinsia ya kiume. Vilevile, anaonekana kuwa 'mwasi' kwa vile anapinga maendeleo ambayo yalikuwa yashapatikana katika kuleta usawa wa mahusiano ya kijinsia na hata kupinga tamaduni ambazo zimekuwepo. Vilevile, anapinga jukwaa lolote lenye uwezo wa kuleta usawa wa kijinsia na hata kuona kuwa mwelekeo huu utamfanya mwanamume kuwa na tabia za kike. Matokeo ya uchambuzi wetu yamepatikana baada ya kuchambua jumbe za @Amerix kwa kutathmini usawiri wa mwanamke, kutathmini mahusiano ya kimamlaka katika misingi ya kijinsia na kuonyesha kiwango cha ama umbali ambao mfumo dume umesonga na hata kujibu swali la ikiwa wanawake na wanaume ni tofauti kwa sababu za Kibayolojia ama tofauti zao zinatokana na maoni ya jamii, haya yakiwa ni kati ya majukumu ya uhakiki wa kifeministi kwa mujibu wa Barry (2009, uk.128). Tunaunga mkono maoni ya Joss Whedon kuhusiana na usawa wa kijinsia kuwa, "Usawa si dhana. Si jambo ambalo tunafaa kung'ang'ania kupata. Usawa ni kama mvutano. Tunafaa kusimama katika dunia hii kama wanaume na wanawake na udunishaji wa mwanamke uliopo katika kila jamii si sehemu ya kweli ya hali ya mwanadamu." Kutokana na utafiti huu, tunapendekeza watafiti wengine wachunguze majukwaa mengine ya mtandao wa kijamii yanavyoshughulikia suala la jinsia, uana na ngono. Aidha, wanaweza kuchunguza masuala ya wanawake tofauti na sisi tulioshughulikia kukwezwa kwa wanaume. Vilevile, wanaweza kutoa suluhu la suala la udunishaji wa jinsia moja.

MAREJELEO

Barry, P. (2009). Beginning Theory: An Introduction to Literacy and Cultural Theory (3rd edition). Manchester, England: Manchester University Press.

Beauvoir, S. (1949). The Second Sex. London, United Kingdom: Pan Book Publishers.

Chiramaoke, I. (2005). Ashawo Suppose Shine Her Eyes': Female Sex Workers and Sex Work Risks in Nigeria. Health, Risk and Society, 7 (2): 141-60

DiYanni, R. (1995) Critical Perspectives: Approaches to the Analysis and Interpretation of Literature. New York, United States of America: McGraw-Hill

Kibigo, M. L. (2020) "Ubabedume katika majigambo ya miviga ya Shilembe na Mchezasili wa Mayo miongoni mwa Waisukha nchini Kenya kwa mtazamo wa kisemantiki." Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro. (Haijachapishwa)

Kimondiu, D. K. (2019). "Usawiri wa mwanamke katika nyimbo za sifo za Wakamba." Tasnifu ya uzamili, Chuo kikuu cha Machakos. (Haijachapishwa)

TUKI, (2004). Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Nairobi, Kenya: Oxford University Press.

Osoro, G. (2003) "Uhakiki wa riwaya za Said Ahmed Mohamed katika misingi ya Kifeministi." Tasnifu ya uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Wafula R. M na Njogu K. (2007). Nadharia za Uhakiki wa Fasihi, Nairobi, Kenya: Jomo Kenyattta Foundation

Wamitila, K. (2002). Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake. Nairobi, Kenya: Phoenix Publishers

Wamitila, K. W. (2003). Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia, Nairobi, Kenya: Focus Publishers. Mtandao

https:///www.inhersight.com/blog/insight-commentary/quotes-from-men-about-genderequality

https:///www.X@amerix

https://youtu.be/882hqwDD8FU (Hotuba ya Rais wa Kenya katika sherehe za Madaraka

01/06/2022)